Unafanya Nini Hapa?

Asante, Ndugu Neville. Kama nilivyosema, asubuhi ya leo, daima ni vyema kuja katika nyumba ya Bwana.

2 Kidogo nilikuwa nawazia kumwita msichana mdogo hapa, usiku wa leo, kuimba wimbo ambao nilimsikia akiimba nyumbani kwangu, hivi majuzi. Naamini tungali tuna wakati kwa ajili yake, ikiwa hajarudi nyuma sana. Binti Jefferies, unafikiri nini kuhusu huo, ule wimbo mdogo ulioimba kule? Niliingia nikasikia ukiimbwa, nami nikaupenda sana. Nami natumai sikuaibishi, kukuomba uuimbe tena. *Niambie Jina Lake*, ama kitu kama hicho. Huo ndio? Ningependa kuusikia tena. Najua nyote mtaufurahia.

3 [Sehemu tupu kwenye kanda. Dada Jefferies anaimba *Niambie Jina Lake Tena*—Mh.]

4 Loo, ninaupenda huo sana! Nalipenda Jina Lake. Je, mnajua kilichonifanya niuwazie huo, kumfanya maskini msichana huyo kuuimba? Yeye ni maskini rafiki msiri shuleni wa msichana wangu mdogo, Rebekah. Nami nilikuwa nimerudi, majuzi asubuhi, nikifanya jambo fulani chumbani, nami nikasikia uimbaji huo. Ndipo nikawazia, "Vema, nitamfanya tu aimbe huo kanisani siku moja."

5 Nikishuka njiani, niliwapeleka watoto shuleni, nami nilizungumza naye kuhusu uimbaji huo. Naye akasema, "Niliamka tu . . . " Huenda nisitumie maneno yale yale kulisema. Lakini alisema, "Niliamka hivi majuzi usiku, ama, nami nilikuwa kitandani, na nilikuwa nikiuwazia wimbo huo, ndipo nikapata kubarikiwa sana!"

6 Vema, nikawazia, "Hilo ni zuri sana, kwa msichana tineja, kuzungumza kuhusu Roho Mtakatifu kuwabariki, hasa katika jamii hii, katika mji huu." Tunahitaji wasichana matineja zaidi kama huyo. Tunawahitaji.

7 Msichana huyu mwingine mdogo ambaye ameimba hivi punde, pia, hapa, dakika chache zilizopita. Sijui jina lake, lakini nawafurahia watoto hao wadogo, wasichana wadogo matineja, wakiimba. Je, mnajua, mwenendo tunaoenenda unakuwa kielelezo kwa wengine? Ndivyo kabisa.

8 Hadithi ya zamani ya miaka kadhaa iliyopita, huko Uingereza, kulikuwako na mtu. Alifikiri angetoka nje akanywe kinywaji kidogo cha kirafiki kwenye msimu wa Krismasi, kwa ajili ya ushirika tu. Basi akaenda miongoni mwa jirani zake naye alikuwa akibadilisha zawadi, na kila mtu angemwambia, "Sasa, Yohana, kunywa tu hiki." Basi kionjo kidogo *hapa* na kionjo kidogo *pale*, ndipo akalewa kwelikweli.

9 Basi akienda zake nyumbani, kulikuja theluji, kama inchi sita. Na—naye mvulana wake mdogo alikuwa akimfuata. Asingeweza kumbeba; alikuwa amelewa kupita kiasi. Basi alikuwa akienda zake nyumbani, ndipo ikawa aligeuka akamwona maskini mvulana wake karibu anagaagaa kwenye theluji. Naye akasema, "Mwanangu, kwa nini unagaagaa katika theluji?"

10 Akasema, "Baba, ninajaribu kufuata nyayo zako." Ndipo akamchukua huyo mvulana mdogo mikononi mwake, na kusema, "Mungu, tangu leo hii na kuendelea, sitakunywa tena."

11 Mtu fulani atafuata nyayo zako. Hebu tutembelee mstari huo mnyofu, tangu utotoni hadi Kalvari. Hizo ndizo nyayo za miguu; hebu tuwe nazo za kutembelea.

12 Sasa, najua usiku wa leo ni usiku wa ushirika. Nami nitakuwa na muda mfupi tu wa kusema nanyi katika Neno. Nami na—napenda kuzungumza juu Yake, kwa sababu Yeye ni halisi sana kwangu.

13 Nilikuwa nikisoma makala kidogo siku moja, nikiwazia juu ya wasichana tena. Ilitukia huko Magharibi. Kulikuwa na usiku mmoja wa dhoruba iliyovuma, nao upepo ni mkali. Basi kulikuwako na watu fulani waliokuwa na mkutano wa maombi. Naye aliyeuongoza huo mkutano wa maombi alikuwa msichana anayevutia sana. Bila kufikiria juu ya hatari ambayo ingemkabili, lakini aliishi pembeni mwa mji huo mdogo. Na kwa kawaida mitaani kulikuwa na watu wengi wakati huo wa usiku. Mkutano wa maombi ulipomalizika, nyimbo zao zilikuwa kwa Bwana, na mioyo yao ilikuwa na furaha. Nami nadhani, kwa jumla, walijisikia kama vile Ndugu Beeler alivyojisikia muda mfupi uliopita alipokuwa akitoa ushuhuda. Walikuwa na furaha tele, wasingeweza kuizuia hiyo shangwe, ndipo ikawabidi kuiachilia tu ijitokeze kwa namna fulani. Baada ya "amina" ya mwisho kusemwa, wote walielekea nyumbani mwao.

14 Basi maskini huyo msichana, alichukua koti lake, na kuinua ukosi juu, na kulifunga mbele yake, akaingia mtaani. Ndipo akaja kugundua kwamba huo usiku wa baridi ulikuwa umemkimbiza kila mtu mekoni mwao. Basi akajikuta peke yake mitaani. Ndipo ikaonekana kana kwamba hatari ilianza kumwandama.

15 Mnajua, nina furaha sana kwamba Roho Mtakatifu anaweza kutuonya kuhusu mambo yajayo; kuepuka hatari hizo.

16 Naye kamwe hakuwa amewahi kuwazia kuhofu. Basi akaanza tu kuimba wimbo ule wa kale: *La, Kamwe Si Peke Yako*. Ndipo wakati akipitia humo mjini, ilionekana kana kwamba hakuna mtu atakayemsumbua, lakini kwa ghafla ikazuka ile hofu kuu tena. Ndipo ikawa aliangalia, akamwona mtu mwenye sura mbaya sana amesimama karibu naye, amemkazia macho moja kwa moja, ameweka mikono yake namna *hii*, akimjia.

17 Hakuna njia ya kutoroka. Na ni hadithi ya kweli. Kwa hiyo asingeweza kutimua mbio; angemshika. Kulikuwako na jambo moja tu la kufanya. Asingeweza kupiga mayowe. Upepo ulikuwa ukivuma vikali, nusura uunyanyue mwili wake kutoka mtaani. Kamwe asingeweza kumfanya mtu yeyote kusikia. Nayo theluji inapofusha tu.

18 Basi kuna jambo moja tu la kufanya, hilo lilikuwa ni kuomba. Kwa hiyo akaanza, chini ya sauti yake, akimnong'onezea Mungu maombi. Naye akasema, hakujua kamwe alikotokea, lakini, kwa ghafula, kando ya mlango, alisimama mbwa mkubwa mno. Naye alikuwa ameinua nywele zake juu, naye akaenda kando yake, na akaja upande ambao huyo mtu angekuwa, na kuanza kunguruma vikali sana, alipokuwa akipita karibu na mtu huyo. Basi mara mtu huyo aliposhuka barabarani, huyo mbwa aligeuka akarudi na kujilaza mlangoni.

19 Mungu atawashughulikia walio Wake. Mungu, wakati mwingine, Yeye hufanya kazi kupitia hata kwa mbwa au mnyama, au njia nyingine, kuonyesha utukufu Wake na ulinzi Wake. Nina furaha sana kwamba ninamjua katika msamaha wa dhambi zangu, na kwa uhakika kwamba dhambi zangu ziko chini ya Damu, ninapoziungama kila siku Kwake.

20 Asubuhi ya leo, katika Ujumbe huu, huenda kidogo nilionekana mwenye kukatakata ama fidhuli, lakini sio sana sana somo la ibada ya u—uponyaji. Lakini nimeishi muda mrefu vya kutosha kujua jambo hili, Ndugu Tony, kama mtu atafanya tu jinsi anavyohisi kuongozwa kufanya, Mungu alishughulikia hayo mengine, kwa njia kuu. Mara ya kwanza ilipopata kutokea namna hiyo, hapa. Kwa kawaida sisi husambaza kadi za maombi, na kuwasimamisha watu. Lakini Roho Mtakatifu alinifanya niulize ni wageni wangapi waliokuwa humo jengoni, ambao wangelijaza kabisa. Ndipo akawafahamisha shauku zao. Na. . . na kutangaza uponyaji wao na kadhalika. Inaonyesha tu, kwamba, "Kutii ni bora kuliko dhabihu, kuwasikiliza. . . na mafuta ya kondoo dume."

21 Kwa hiyo, usiku wa leo, nimechagua Maandiko madogo hapa kwa dakika chache tu, kuzungumzia. Na kabla hatujafanya hivyo, hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi tu katika maombi.

22 Bwana, Wewe ndiwe Mungu, hata milele. Nasi tunakushukuru na kukusifu Wewe kwa ajili ya majaliwa tuliyo nayo, ya kuja mbele Zako, katika njia ya maombi. Tukijua hili, kwanza, ya kuwa tumeahidiwa, ya kwamba, "Mkiniomba lolote katika Jina Langu, nitalifanya." Nasi tuna hakikisho ya kwamba utatutimizia haja yetu.

23 Basi kuna mengi sana ambayo tayari yamefanywa, usiku wa leo, hata tunajisikia kwamba kama tungefunga tu ibada

na kwenda nyumbani, tungeweza kusema, "Imekuwa vizuri kuwa hapa." Kusikia nyimbo hizi za Sayuni, zilizoimbwa katika hili kusanyiko! Kuwasikia watu wanapotoa sauti zao katika maombi, na katika kutafakari, na katika tenzi! Kama Maandiko yasemavyo, "Mkifanya shangwe moyoni mwenu, mkiimba nyimbo za kiroho." Kuwasikia wasichana hawa matineja! Katika saa hii yenye giza, kama ilivyoelezewa usiku wa leo kupitia kwa Ndugu yetu Beeler, tunayoishi ndani yake, na kuwasikia wakiimba nyimbo za Sayuni! Kusikia maelezo ya Ndugu Beeler Kwako, jinsi alivyokuthamini, na yale uliyokuwa umefanya, na jinsi ulivyomlemaza, kumfanya atambue angefanya nini bila mkono huo sasa. Inaonyesha tu kwamba tunalindwa na neema na nguvu Zako.

24 Hebu sote tutahadhari, usiku wa leo, Bwana. Kwa maana, ninaamini kuwa ni wakati wetu wa kufanya hesabu, wakati wa kujichunguza, kwa maana hatujui wakati wa kuondoka utakuwa lini. Huenda ikawa imechelewa kuliko tunavyodhania. Kwa hivyo na tuzingatie njia zetu, usiku wa leo, na mawazo yetu.

25 Nasi tungeomba ya kwamba ungesema nasi kwa dakika chache katika Neno, kisha utubariki katika ibada ya ushirika baadaye. Tunapokula vipande vilivyovunjwa-vunjwa vya mkate huu mwembamba, na divai, ambavyo vinawakilisha mwili Wako uliovunjwa na Damu iliyomwagika, kwa ondoleo la dhambi zetu.

26 Mchungaji wetu mpendwa sana, usiku wa leo, hakuwa anajisikia vizuri sana. Lakini, katika mazungumzo yetu ya simu, ameliweka madhabahuni. Nina hakika utalipokea, Bwana. Na tena ninamwombea, kwa maana tunampenda na tunamhitaji. Tunamwombea yeye na familia yake, na kwa ajili ya kila familia iliyoko hapa, na kwa ajili ya maombi yote yaliyonenwa usiku wa leo, na yaliyo kimya, pia.

27 Utubariki zaidi mikutanoni. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu, Mwanao. Amina.

28 Ninataka kusoma sehemu ndogo tu ya Maandiko hapa, inayopatikana katika Wafalme wa Kwanza 19, na kuanzia kifungu cha 9.

> *Akafika kunako pango, akalala ndani yake; na, tazama, neno la* B*WANA* *likamjia, na . . . akamwambia, Unafanya nini hapa, Eliya?*
>
> *Akasema, Nimekuwa na* bidii ama *wivu mwingi kwa ajili ya* B*WANA* *Mungu wa majeshi:* na *kwa kuwa wana* wake *wa Israeli wameliacha agano lako, na kuzivunja madhabahu zako, na kuwaua manabii wako kwa upanga; nami, mimi* peke yangu, *nimesalia; nao wanaitafuta roho yangu, waiondoe . . .*
>
> *Akasema, Toka, usimame mlimani mbele za* B*WANA*. *Na, tazama,* B*WANA* *akapita, upepo mwingi wa* dhoruba

> kuu ukapita na *kupasua* mlima, *ukaivunja-vunja miamba mbele za* B*WANA; lakini* B*WANA hakuwamo katika upepo ule: na baada ya upepo tetemeko la nchi; lakini* B*WANA hakuwamo katika tetemeko hilo:*
>
> *Na baada ya tetemeko la ardhi*. . .*moto; lakini* B*WANA hakuwa katika moto ule: na baada ya moto sauti ndogo tulivu.*
>
> *Ikawa, Eliya aliposikia, akajifunika uso wake katika vazi lake, akatoka, akasimama* mlangoni *mwa pango. Na, tazama, sauti ikamjia, kusema, Unafanya nini hapa, Eliya?*

29 Ninataka kuchukua kama somo, kwa dakika chache: *Unafanya Nini Hapa?*

30 Eliya alikuwa na siku ngumu. Alikuwa juu ya Mlima Karmeli, naye alikuwa ameuona utukufu wa Bwana ukishuka. Alikuwa ameomba moto kutoka mbinguni, na—na kisha akaomba mvua inyeshe juu ya nchi. Na chini ya uchovu huu wote, mishipa yake ilikuwa karibu kupasuka. Loo, jinsi ninavyoweza kumhurumia!

31 Na hapa tunamwona, kwanza, akilihubiri taifa la watu waliorudi nyuma. Na kwa Yezebeli aliyetaka kufanya atakavyo. Nao watu walikuwa wamefikia mahali ambapo walikuwa wamemwacha Mungu, wakaziacha ahadi Zake zote na amri Zake zote, wala hawakuzishika tena sheria Zake, wala hawakumjali Yeye. Naye Eliya, katikati ya hayo yote, asingeweza kupatana. Ilimbidi kusimama mwaminifu kwa imani yake. Loo, jinsi hilo linavyoakisi katika siku hii!

32 Nao walikuwa na malkia pale, jina lake Yezebeli. Naye alikuwa amewapotosha wana wa Israeli wote, kwa njia yake ya kisasa ya maisha ya ajabu. Aliwasababisha kufanya uasherati na kufanya mambo maovu. Kama hiyo si mfano mzuri wa siku hizi!

33 Lakini, Eliya, katikati ya hayo yote. . .Hata hivyo, wengi wa wana wa Israeli, maelfu yao, walikuwa wamepatana, nao walitaka kuishi maisha ya mtindo wa kisasa. Hata hivyo, Eliya asingepatana. Alimwambia Yezebeli mahali pake na jinsi anavyopaswa kufanya. Loo, alimchukia nabii huyo. Lakini, hata hivyo, asingemdai, bali alikuwa mchungaji wake.

34 Loo, kuna nyakati nyingi hawataki kudai hilo, lakini mtu aliyetumwa na Mungu kwa jamii ni mchungaji wa hiyo jamii yote, kama yeye ni Mbaptisti, Mpresbiteri, au ni nani. Mungu humtia mafuta mtu Wake, wala hatapatana. Nao watu wakati mwingine humchukia, kwa sababu kwamba anaitetea Kweli, lakini hata hivyo yeye ni mchungaji wa Mungu kwa ajili ya wakati huo.

35 Loo, alimdharau. Angefanya lolote awezalo kumwua, lakini hata hivyo alikuwa mwaminifu kwa kanuni za Mungu na

viwango vya Mungu. Karamu zake za kisasa na vilabu, na kuupodoa uso wake, na uvaaji wa nguo zake, ulikuwa umelichafua taifa hilo. Naye mzee Eliya hakuwa rahisi. Alimwambia pale pale alipokuwa amesimama.

36 Mungu na atutumie Eliya wengine zaidi katika siku hizi, ambao hawataridhiana na dhambi; mtu ambaye ataihubiri Kweli, haidhuru inaumiza jinsi gani. Mungu angali ana watumishi katika kila jamii, ambao hawatapatana na mambo ya ulimwengu.

37 Eliya hakupenda mtindo wa kisasa wa mambo, kwa hiyo alisimama mwaminifu kwa Mungu. Ndipo pambano la kuamua likatokea. Nayo makabiliano ya kuamua yamekuja tena.

38 Naye Eliya, juu ya Mlima Karmeli, walipodhania ya kwamba siku zote za miujiza zilikuwa zimepita, wala kusingekuwako na kitu kingine kama miujiza, kulikuwa na mtu mmoja ambaye aliiamini. Naye akasema, "Walete manabii wenu wote. Waleteni hapa juu mlimani, na hebu tuthibitishe tuone Mungu ni nani." Napenda Andiko hilo.

39 Loo, kama kuliwahi kuwa na wakati, mahali fulani, ambapo Nguvu za kweli za Mungu zinapaswa kudhihirishwa, ni leo hii. Hebu tuthibitishe Mungu ni nini.

40 Ikiwa elimu ndiyo njia ya kupata uhuru, kwa nini isichukue hatua? Ikiwa misimamo ya kijamii, na kadhalika, ndiyo njia ifaayo, kwa nini isichukue hatua? Kama kuyalipa mataifa mengine kuwa marafiki zetu...Nasi tunaona wanatugeuka, mara tu wawezapo. Wala huwezi kununua urafiki kwa pesa. Urafiki ni karama ya Mungu. Ikiwa makanisa makubwa na waalimu wakuu ndio njia ifaayo, kwa nini tusiwe na Mungu zaidi katika jamii zetu basi? Kwa nini sikuzote tunazidi kurudi nyuma? Ikiwa mpango wa elimu, na mimbara iliyofunzwa vizuri, na kwaya iliyofunzwa vyema, na sikuzote tunazidi kwenda mbali zaidi na Mungu, wakati wote, basi haitafanya kazi.

41 Sayansi imefanya nini? Sayansi, mnasema, "Wakati utakuja ambapo sayansi inaweza kufanya *hivi* na kufanya *vile*." Wamefanya nini? Wametufikisha mahali ambapo wanaiangamiza dunia nzima. Wanafanya nini? Wanaiharibu dunia badala ya kuiboresha.

42 Si muda mrefu uliopita, wakati Kapteni Al Farrar wa FBI, juu ya sehemu za vijana za Marekani, alipokuwa nami ofisini mwake; nikiisha kumwongoza kwa Kristo, chini kwenye mahali pa mazoezi ya kupiga bunduki. Alisema, "Ndugu Branham, mimi ni Mbaptisti. Nasikia ulikuwa Mbaptisti."

Nikasema, "Naam, bwana."

43 Akasema, "Lakini sina Roho Mtakatifu huyo unayezungumzia." Akasema, "Unafikiri angekuwa ni kwa ajili yangu?"

Nikasema, “Naam, bwana.”

44 Akasema, “Vema, nitaagiza chumba kizuri mahali fulani katika chumba kizuri cha hoteli. Ndipo mimi na wewe twende kule, na labda Yeye atakuja kwenye hicho chumba cha hoteli na kunijaza na Roho Wake.”

Nikasema, “Huna ho-...si lazima uwe na chumba cha hoteli.”

Kasema, “Vema, angekutana nami wapi?”

Nikasema, “Papa hapa.”

45 Akasema, “Asingekuja mahali hapa pa kupigia bunduki, sivyo, mahali pa kupigia bunduki hapa?”

46 Nikasema, “Alikwenda katika tumbo la nyangumi kwa ajili ya mmoja; ndani ya tanuru ya moto kwa ajili ya mwingine. Atakutana nawe kwa misingi yoyote ambayo utakutana Naye.” Hakika. Mungu anataka kukutana nawe. Anataka kulizungumza nawe. Atakuja mahali ulipo.

47 Sasa, Yezebeli alikuwa ameichafua nchi. Naye Eliya alikuwa amefadhaika sana, naye alikuwa amefanya miujiza mikubwa sana na kufanya ishara huko kwenye kilima, kuthibitisha kwamba Mungu alikuwa angali ni Mungu, na angeweza kujibu kwa njia ya mwujiza. Nalo lilisababisha nini, matokeo? Tishio kwa maisha yake mwenyewe. Ilisababisha nini badala ya uamsho wa ulimwengu wote? Ilisababisha tishio kwa maisha yake.

48 Yezebeli, wakati Ahabu alipomwambia mambo haya, alisema, “Miungu na wanifanyie, na zaidi, pia, nisipokikata kichwa chake kufikia wakati huu kesho usiku.”

49 Naye Eliya aliyekuwa akijaribu, pamoja na moyo ndani yake, wa Mungu, akijaribu kuwaonyesha watu ya kwamba Mungu alikuwa angali ni Mungu. Nalo likamwendea kinyume. Ndipo akakimbilia nyikani aliposikia hayo. Na hapo akalala chini ya mretemu, akijaribu kupata faraja. Alikuwa—alikuwa amemwondosha mtumishi wake, akamwacha.

50 Sasa, hadithi yetu inakwenda katika sehemu tatu mbalimbali. Moja, Mlima Karmeli; inayofuata, chini ya mretemu; na sehemu ya tatu Mungu anapokutana naye, yuko pangoni.

51 Na ni ajabu sana. Mchungaji hapa anajua, na wahudumu wengine. Angalieni, baada ya Milima Karmeli yako, utakuwa na mretemu. Wakati wowote mtu anapokuwa na baraka, na Nguvu za Mungu zinamiminika na kukufanyia jambo fulani, tahadhari, Shetani yuko njiani. Kumbukeni tu, kesho yake, Jumatatu hiyo baada ya siku njema Jumapili, litakuwa ni jambo gumu, kwa sababu atafanya kila awezalo kuishambulia imani hiyo kutoka kwako, ambayo Roho Mtakatifu alitia ndani yako hivi majuzi.

Kwa hiyo, Eliya alikuwa na siku kuu. Naye ana wasiwasi, kwa vyovyote vile.

52 Manabii wote wana . . . walitangazwa kuwa wendawazimu. Yesu Kristo alitangazwa kuwa mwendawazimu. Kila mmoja wa mitume alitangazwa kuwa ni mwendawazimu, na umma, maana huduma yao ilikuwa ya kimbinguni sana hata watu wakafikiria wamerukwa na akili. Kila mtu anayeishi kwa utauwa katika Kristo Yesu atapata mateso. Unakuwa mtu tofauti.

53 Kama vile Ndugu Beeler alivyosema kuhusu ishara yake huko nyuma, unazaliwa mara ya pili. Unakuwa kiumbe kipya katika Kristo. Mambo ya kale yamepita. Mambo ya kimwili ya ulimwengu hayana nguvu tena juu yako, wala wewe huyashikilii tena, wakati umepita kutoka mautini kuingia Uzimani.

54 Mungu anapomshika mtu, jambo la kwanza analofanya kanisani ni kulitoa katika mambo ya kilimwengu liingie kwenye utakatifu, ndipo analitoa kutoka mautini kuingia Uzimani. Linazaliwa mara ya pili. Ni jipya. Mawazo yake ni mapya. Tunachohitaji ni uamsho kama huo, leo hii. Ni kweli hasa. Loo, tumekuwa na kuzamishwa kwa Roho. Tumekuwa na baraka za kiroho na misukosuko ya kiroho, lakini hatuhitaji hayo tena. Tunahitaji uamsho wa Roho wa Mungu aliye hai, mioyoni mwa watu. Hatuhitaji kuzamishwa kwingi kwa Roho, au uamsho wa kiroho. Tunahitaji uamsho, hiyo ni, kuamsha yale tuliyo nayo. Si uamsho wa kiroho; wakati mwingine huo husababisha umati uliochangamana mno. Lakini tunahitaji uamsho ambao utapepeta chini, utikise chini, na utakatilia mbali mambo yote.

55 Kama vile kusimama karibu na ufuo wa bahari. Nilikuwa nikizungumza na baadhi ya ndugu huko Puerto Rico majuma machache yaliyopita. Kwamba, nilipoiona ile bahari kuu, na dhoruba kuu, mawimbi yalikuwa marefu kuliko maskani hii. Nami nikasema, "Mnajua nini? Haina tone moja zaidi la maji ndani yake kuliko wakati imetulia kabisa. Lakini, je, huko kuvurugika na kuruka-ruka, nako kunamaanisha nini? Kunatupilia mbali takataka zote kutoka kwake, ukingoni."

56 Hicho ndicho Kanisa linachohitaji, ni uamsho, kutikisa kutoka Kwake malimwengu yote na mambo ya ulimwengu, na kurudisha usafi na utakatifu wa Mungu, mioyoni mwa waaminio Wake, unyenyekevu.

57 Mbona, watu, kujiridhisha wenyewe, wasipopata uamsho mara moja moja, rohoni mwao, wanakuwa wa kimwili sana na wasiojali sana, mpaka wanakuwa na ubinafsi, wagumu, wenye kiburi sana. Wanasoma na kujifunza, na hilo ni sawa, lakini hilo silo jambo tunalozungumzia. Unajua zaidi kuhusu Neno. Ni vizuri kujua Neno, lakini ni bora zaidi kumjua Mwandishi wa Neno. Unaona? Maskini kitu Fulani hicho unachopuuza, kitu Fulani hicho moyoni kinachokufanya jinsi ulivyo, kitu ndicho hicho.

58 Nami nawaambia, Eliya, na huku amefadhaika sana, kwa vyovyote vile, sikuzote nilimhurumia, moyo wake ulikuwa karibu kuvunjika, kwa vyovyote vile, nalo pigo hilo kubwa kutoka kwa Yezebeli lilimalizia mapigo yake. Ndipo akatoroka, akaenda nyikani akajilaza chini ya mretemu.

59 Loo, ujuzi huo wa mretemu! Kuna wengi wetu tunaojikuta chini ya mretemu. Ninajipata mwenyewe chini pale, mara nyingi, kufikia mahali ambapo hujui la kufanya. Umechanganyikiwa. Kusema kweli, niko chini yake sasa, na ninashangaa, "Ee Mungu, ungetaka nifanye nini?"

60 Unajua, watu walio chini ya mretemu ni kama Eliya, wanapenda kulala. Ni—ninawahubiria watu waliochoka kuliko mtu yeyote ulimwenguni. Watu wamechoka sana. Wa—wa—wa—wamesongwa akili sana mpaka wanazijaza taasisi za wendawazimu na hospitali, kila mahali. Wameshikwa na wasiwasi sana hata hawajui wanachoamini, wala wanachotaka. Wanalala tu pale. Hawajui la kufanya. Loo, ni tamasha ya kusikitisha sana.

61 Sikiza hapa, ndugu yangu. Huwezi kuutuliza kwa kunywa pombe. Huwezi kuupigia kelele uondoke. Wala kuuchezea karata hata utulie. Nawe ungeweza kulala usingizi wa mchana mara elfu ukijaribu kuuondoa kwa usingizi, wala huwezi kufanya hivyo. Maskini tiba zetu zote, jambo pekee zinalofanya ni kuzichochea hizo dalili. Hatuna budi kuwa na tiba ya huo ugonjwa. Hatuna budi kuwa na . . . Madaktari wote wa magonjwa ya akili ulimwenguni hawawezi kuutibu huo. Inasaidia tu zile dalili. Tiba iko katika Damu ya Yesu Kristo. Sio kupumuzikia ufukoni mwa bahari. Si kuimba wimbo wa taifa, kwaya ya kuimba nyimbo za taifa. Hilo ndilo tunalojaribu kufanya, siku hizi, kuumaliza kwa uimbaji.

62 "Loo, tutajifanya kama akina Jones." Nasi tu—tunajaribu kufanya jambo tofauti, kujaribu kuumaliza kwa elimu. Kuna njia moja tu ya kulifanya, hiyo ni, kukabiliana na ukweli wa mambo. Hiyo ni kweli. Loo, kama umefadhaika na kuchanganyikiwa, usijiunge na kanisa. Njoo kwa Kristo. Hiyo ndiyo tiba ya pekee. Usitumie na kufungua ukurasa mpya. Pata tu Maisha mapya. Kristo ndiye jibu.

63 Hapo alilala, chini ya mretemu. Hakujua la kufanya. Alikuwa amevunjika moyo. Alikuwa akitetemeka. Alikuwa akilia, bila shaka. Naye alikuwa katika hali mbaya sana.

64 Wengi wetu hufikia nyanda hizo, hasa baada ya tukio la Mlima Karmeli. Niliulizwa, hivi majuzi, na mtu fulani, kuhusu hilo. Na jinsi ambavyo . . . Tungefanya nini . . . Je, tunaweza, sisi, kufanya nini? Tunaweza kufanyiwa nini wakati huo? Kuna jambo moja tu la kufanya: jikabidhi kwa Mungu. Sasa, najua kwamba mtu anaweza kufanya kazi kupita kiasi, na mtu anaweza kuzembea sana, mtu.

65 Mungu alijua mtu huyu anahitaji kulishwa. Alihitaji kitu cha kula. Na chini ya mahali hapa, alipokuwa amelala, ilimbidi Mungu amfanyie jambo fulani.

66 Mungu hana budi kumfanyia jambo fulani kila mtu anayekuja chini ya mretemu, la sivyo atavurugika. Hana budi kufanya hivyo, endapo mtumishi Wake amelala chini ya mti, kule, hajui la kufanya. Ametekeleza agizo lake.

Eliya akasema, "Ee Bwana, niache nife."

67 Nimekuwa na hisia hizo baada ya kutoka kwenye mkutano, na ilionekana kana kwamba nilijaribu, na kuhubiri, na kusihi, na kushawishi, na kumwona Malaika wa Mungu akipitia mkutanoni na kufanya ishara na maajabu. Na kuketi huko nje ndani ya gari, na kuwasikia wakilia, wakisema, "Hiyo haikuwa kitu ila saikolojia. Hamna kitu Kwake. Hamna kitu Hapo. Hayo yote ni upuuzi."

68 Loo, ndipo ninatambaa chini ya mretemu. Nawazia, "Bwana, kwa nini Wewe—kwa nini uliniruhusu kufanya hivyo? Ifanyweje?" Lakini sote hufikia matukio hayo. Lakini, rehema za Yehova, kwa mtumishi Wake! Mungu anajua majaribu yako. Jua tu jambo hili, Yeye anajua yote kuyahusu, kwa hiyo Yeye hushuka.

69 Naye anajua mtumishi Wake anahitaji pumziko, kwa hiyo Yeye humlaza tu usingizini kwa muda kidogo; wakati amelala pale, akingoja kupata nafuu, ama akiomba apate kufa. "Bwana, baba zangu walikufa, mbele yangu, basi sasa utwae uhai wangu. Nimefanya ya kutosha. Nimepiga vita vizuri, mwendo nimeumaliza." Lakini kulikuwa na kazi ya kufanywa bado. Mungu hakuwa amemalizana na nabii Wake. Angali alikuwa na kazi.

70 Haidhuru tunalia kiasi gani, na kuwazia *hili, lile,* ama *linginelo*, hakuna kinachoweza kutuchukua mpaka Mungu amemalizana nasi. Nina furaha sana kujua hilo.

71 Wakati mwingine unajisikia kama, kama nilivyojisikia wakati mmoja, kuilenga bastola kichwani mwangu, nipate kujiiua, lakini nisingeweza kufanya hivyo. Nilitoa glavu yangu, nipate kushika waya za volteji kubwa ambako nilikuwa nikifanya kazi, lakini sikuweza kujiiua. Kitu fulani bado kilishikilia. Mungu yeye yule aliyekuwa pamoja na Eliya, Mungu yuyo huyo, leo hii! Aliniona chini ya mretemu. Mke wangu na mtoto mchanga wamelala kule kaburini; na baba yangu, ndugu yangu, na wote. Nilikuwa karibu nimekwisha, mimi mwenyewe. Nimelala chini ya mretemu. Ni vigumu. Nami nikafika mahali, nilikuwa nimechanganyikiwa vibaya sana, nikajaribu kuifanya bunduki iulipulie ubongo wangu mbali; isingefanya hivyo. Mnaona? Kungali kuna kazi ya kufanywa. Jambo fulani lazima lifanywe. Mungu alikuwa hajamaliza. Sikuzote atakutunza.

72 Maskini, mtumishi mchovu, aliyechoka! Alimwona. Alijua mahali alipokuwa.

73 Anajua ulipo, usiku wa leo. Unaweza kuwa chini ya mretemu, kila kitu kimeenda, lakini, kumbuka, Yeye anajua mahali ulipo. Hatuhitaji lundo la marekebisho.

74 Kama vile maskini yule mwanamke mweusi alivyosema, kule Kusini. Alikuwa amepata ajali; gari lilikuwa limemgonga. Na ilikuwa. . . Lilimwumiza vibaya sana, ndipo—ndipo wakili akasema, "Je, unataka kushtakia uharibifu?"

75 Akasema, "Sheria-ee, rehema! Hapana, mpenzi." Kasema, "Nina uharibifu wa kutosha. Nataka ukarabati kiasi."

76 Nami nafikiri alizungumza vyema kwa niaba ya jamii hii, na kanisa hili, usiku wa leo, na Marekani hii inayoelekea kuzimu. Haijarudi nyuma; tayari imekwisha. Ha—haiko njiani mwake kwenda kuzimu; tayari imekutana na kuzimu. Haijapotea, haitopotea; tayari imepotea. Haina haja ya kushtakia uharibifu; inahitaji ukarabati. Ni ukweli. Anajua ulipo. Anajua mahali umelala.

77 Naye akamtuma Malaika. Naye Malaika akamgusa, ndipo akalala. Naye alipoamka, kulikuwako na ugali wa mahindi, ama aina fulani ya keki, zilizookwa, zimewekwa kando yake. Naye akasema, "Eliya, amka ule." Hiyo hapo neema ya Mungu, kwa mtumishi Wake. Unaona, Yeye anampumzisha.

78 Unajua, Yesu alisema, "Njoni kando, nyikani, na tupumzike kwa muda kidogo." Baadhi ya jamaa hawa ambao wanadhani huna haja ya kupumzika, tunaona kwamba wanaungua haraka sana, pia. Wasipopumzika, wanajikuta wameharibikia mahali fulani. Nafikiri hapo ndipo Ndugu yetu Billy Graham alipo, usiku wa leo, akijaribu kuvuka mpaka. Miili hii ya kibinadamu ina nguvu, lakini inahitaji kupumzika.

79 Halafu unaweza kupumzika kidogo, na kwenda mahali fulani, nao watakukosoa, waseme, "Nilidhani alikuwa mhubiri. Mwangalieni, huko nje ukingoni, akivua samaki," au kitu kama hicho. Lakini hiyo haijalishi. Yehova atawatunza Walio Wake.

80 Ndipo alipokuwa amelala pale, chini ya ule mti, akiwa amechoka na kufadhaika, Mungu aliutuliza moyo wake. Alimlisha. Akamwamsha tena, na kumlisha tena, kisha akamrudisha usingizini.

81 Mnajua, mara nyingi nimeshangaa ni nini kilikuwa kwenye keki hizo. Alipata vitamini ya aina gani kwenye keki hizo? Hata hivyo, chochote kilichokuwamo mle ndani, kilimdumisha siku arobaini mchana na usiku. Alikwenda kwa nguvu za keki hizo.

82 Mungu anajua, usiku wa leo, ninahitaji baadhi yake. Na nina hakika ya kwamba kanisa hili linahitaji baadhi yake. Njoo kando, mbali na ulimwengu, na tupumzike kidogo. Hebu tuzungumze kidogo.

83 Huna muda wa kupumzika, unasema. John Wesley alisema jambo hilo, wakati mmoja. Alisema, "Ninaogopa kupumzika. Sina wakati wa kupumzika." Nawe unajikuta umevurugika, ikiwa hutachukua mapumziko haya.

84 Nasi tunaona, basi, ya kwamba aliendа siku arobaini mchana na usiku, naye Mungu akaona mahali alipokuwa, amesimama, ama amerudi pangoni. Naye Mungu alitaka kuvutia usikivu wake. Kwa hiyo dhoruba kubwa ikapita, nayo ikaipasua milima. Ilikuwa na nguvu sana mpaka ikatikisa miamba, lakini Mungu hakuwa kwenye dhoruba ile. Ilimtangulia Mungu. Ndipo kukaja, tena, tetemeko kuu la ardhi lililoitikisa dunia, lakini, hata hivyo, Mungu hakuwa katika tetemeko hilo. Kisha ukatokea moto, lakini Mungu hakuwa katika moto huo. Ndipo ikaja Sauti ndogo tulivu, naye Mungu alikuwa katika Sauti hiyo.

85 Na, ndugu, dada, nimekuwa pangoni muda mrefu kutosha, nawe, pia, kujua kwamba kumekuwa na matetemeko mengi ya ardhi yanayotikisa pande zote, kelele nyingi na fujo, na mizozo, na mambo kama hayo, na mikutano mikubwa. Lakini Mungu amekuwa wapi, katika hayo? Hiyo ndiyo sababu nilisema niliyosema asubuhi ya leo. Hapana budi litokee jambo lenye kilindi kuliko ibada ya uponyaji. Inabidi kuje kitu chenye kilindi kuliko karama ya kunena kwa lugha. Inabidi kutokee kitu chenye kilindi kuliko upepo mkali ukienda kasi. Upepo ulipita, lakini Mungu hakuwa ndani yake. Tumekuwa na upepo mkali ukienda kasi, kote nchini, na mihemuko, na damu usoni, na mikononi, ishara za kila namna. Lakini Mungu yuko wapi?

86 Eliya alingoja. Hata hivyo, yeye alikuwa nabii, bali aliyasikiliza Hayo. Kamwe hakwenda kulinganisha miamsho na hayo. Hakutoka kwenda kununua hema kubwa kuliko yote nchini. Hakutoka kwenda kwenye televisheni, ama kadhalika, kama vile tungeiita.

87 Mizozo yote mikubwa, nayo Marekani ina hatia ya kusikiliza kelele hizo. Loo, tunapenda kelele, lakini Mungu hayuko kwenye kelele. Ingawa, kadiri zilivyo na heshima na kadhalika, hata hivyo, Mungu hayuko kwenye kelele. Kama hiyo ingalikuwa hivyo, wakati Waafrika walipopiga zile ngoma, kamwe hujawahi kusikia kelele na uwiano wa sauti kama huo. Mungu hakuwa ndani yake. Nasi tumekuwa na upepo mkali ukienda kasi. Tumekuwa na kila aina za mioto, na matetemeko ya ardhi, na kutikisika, na miamsho mikuu, na mambo kama hayo. Mungu hakuwa ndani yake. Kama ingekuwa, ingejitokeza yenyewe.

88 Lakini, baada ya hayo, ikaja Sauti ndogo tulivu, ndipo Mungu akawa katika Sauti hiyo.

89 Hivyo ndivyo ninavyowazia leo, marafiki. Sisi watu tu—tunachukuliwa sana na kelele zote. Kwa hivyo, Marekani inapenda kelele. Angalieni wanachofanya. Wanafungulia maskini redio hizi, kwa nguvu tu wawezavyo, pamoja na roki,

na bugibugi, upuuzi wote wa namna hiyo. Inawabidi kuuwekea sauti kubwa sana, ungevipasua viwambo vya maskio yako, karibu hivyo, kelele zote, siku nzima.

90 Na kanisani, tunapiga matari, tumekimbia huku na huku, na kupiga mayowe na kupiga makelele, na shangwe, na tukawa na wakati mzuri namna hiyo. Hakuna neno dhidi yake, lakini Mungu alikuwa wapi ndani yake? Ilifanya nini? Ilitugawa katika vipande vidogo vidogo, vinavyoitwa Assemblies of God, church of God, Umoja wa Muungano wa Kipentekoste, madhehebu haya mengine yote madogo. Mungu hakuwa ndani yake. Ni mtangulizi wa Mungu. Ni mfumo.

91 Unapoona unaoitwa Ukristo siku hizi, watu wanaoenda makanisani na—na kuishi maisha haya ya kiungwana, nao wanatoka nje na kukana uponyaji, na kukana Nguvu za Mungu, na kukana maisha yaliyowekwa wakfu, wakiwaita "walokole," kumbukeni, huo ni mfumo. Hiyo ni . . . Ndugu Wood, naamini unaiita kazi ya jukwaa. Ni bandia. Ni fremu inayowekwa upande wa nje. Mungu anasimama tu juu yake, kulijenga jengo. Utukufu kwa Mungu! Ni fremu tu ya bandia itakayobomoka.

92 Tumepiga makofi, na kusema, "Utukufu kwa Mungu! Ukipaza sauti, umempata." Wamethodisti walisema hivyo, Wanazarayo. Wakagundua kuwa hawakuwa Naye.

93 Pentekoste ilisema, "Piga makofi na upaze sauti, mpaka unene kwa lugha. Umempata." Lakini tuligundua hatukuwa Naye.

94 Kuna jambo moja zaidi lililosalia. "Basi, Mungu, nipeleke pangoni ambako ninaweza kuipata." Hebu tuipate Sauti hiyo ndogo tulivu, Kitu fulani hicho kinachotia ubora maishani. Hicho Kitu fulani, ambacho, "Ujaponena kwa lugha za wanadamu na Malaika, wala huna Hicho, si kitu wewe. Ujapotabiri na kunena kwa lugha, na kuonyesha ishara na maajabu, na kufanya miujiza na kufanya ishara kubwa, lakini, kama hiyo Sauti ndogo tulivu haiko ndani humo, si kitu wewe," yasema Maandiko. Hiyo ndiyo tunayoisikiliza sasa.

95 Tumekuwa na ngurumo. Tumekuwa na moto. Tumekuwa na upepo ukienda kasi na matetemeko ya ardhi. Lakini, "Mungu, tutumie ile Sauti ndogo tulivu." Hiyo ndiyo tunayohitaji. Sikiliza, ndugu. Tunahitaji hiyo Sauti ndogo tulivu, Sauti ndogo tulivu iliyonena.

96 Yesu. Alisema, "Usingeweza kuisikia Sauti Yake njiani. Hukumsikia akilia." Alikuwa kielelezo chetu. Mwangalieni Yeye. Alifananishwa, Roho Yake, kama hua, mpole.

97 Vitu vikubwa ndivyo vitu vitulivu. Mlijua hilo, marafiki? Sikilizeni. Jua, ambalo huleta uhai juu ya nchi, kwa kila kiumbe hai, katika maisha ya mimea, uhai wa mimea, maisha ya miti, yoyote yale, huleta uhai, jua huuleta. Nalo linaweza kuvuta galoni milioni moja za maji kutoka duniani, na kufanya

kelele kidogo kuliko tunvyoweza kuchota ndoo moja iliyojaa kutoka kwenye pampu. Mnaona? Ni vitu vikubwa. Vitu vitulivu ndivyo vitu vikubwa. Umewahi kusikia dunia ikipinduka? Je, umewahi kusikia sayari zinapopita kwenye mizingo? Umewahi kusikia moja? Hivyo ndivyo vitu vikubwa. Umewahi kusikia jua likichomoza?

98 Loo, tunafikiri tunapaswa kuwa na kelele nyingi sana, tunapaswa kuwa na bendi ya shaba, kuicheza, kurukaruka kwingi sana juu-chini, la sivyo hatuna mkutano mzuri. Tunafikiri kila mtu anapaswa kuwa juu kabisa, wanapiga makofi na kadhalika. Tunafikiri muziki hauna budi kuwa unaendelea katika uwiano wa sauti, na kila mtu akimbie huku na huku kwenye marefu ya kanisa. Tumekuwa na hayo. Imeleta faida gani? Iko wapi? Imetufikisha wapi leo hii? Katika lundo la machafuko, lundo la madhehebu; yaliyofarakana, udugu umeharibiwa. Bila shaka, umeharibika. Imekuwa yule parare wa kale, na tunutu, na—na kila aina ya mende kutoka huko nyuma mwanzoni. Naye Ayubu aliona, ama. . . Yoeli aliwaona. "Kilichosazwa na tunutu, kimeliwa na parare; na kilicholiwa na parare, kimeliwa na nzige," na kadhalika, mpaka tumeula kufikia kwenye kisiki.

99 Lakini Maandiko yanasema, "Nitarudisha, asema Bwana." Tunangojea kitu fulani.

100 Baina ya hizo kelele zote, tumekuwa na mlipuko wa kutosha pamoja na kelele za kutosha ku—kuuongoa ulimwengu mzima. Tumekuwa na shangwe za kutosha na mayowe na makelele. Mpaka, yamefanya nini? Hayajalijenga Kanisa. Yamejenga madhehebu. Yamewafanya watu watoke wakiwa na mawazo ya kiburi na majivuno. Sipendi upuuzi huo. Kuingia jukwaani, waseme, "Loo, mwangalie. Yeye ni mtawala. Angalia jinsi alivyovalia, amenadhifika kweli na kila kitu. Anajua jinsi ya kupanga vokali zake, na kadhalika." Hao sio wale Mungu anaowachagua.

101 Nabii mmoja aliwaza hilo, siku moja. Alikuwa anaenda kumtia mafuta mtumishi. Akasema, "Yeye ndiye mkubwa zaidi katika familia. Ataonekana sawa." Lakini Mungu akamkataa.

102 Sio lazima uwe na watawala, na—na kadhalika, kusimama pale kama sijui-nini. Si mavazi unayovaa, au unavyozungumza kwa ufasaha. Ni kitu Fulani kilicho ndani yako, Sauti hiyo ya Mungu. Hiyo ndiyo.

103 Huyo nabii akapitia karibu na mwingine, kasema, "Huyo siye. Mungu amemkataa." Akampita mwingine. Kasema, "Kwani huna mwingine?"

104 Kasema, "Tunaye maskini mtoto mwekundu, huku nyuma ubavuni mwa kilima, akichunga kondoo." Ilikuwa ni Daudi.

105 Walipomleta maskini jamaa huyu mdogo mwenye nywele nyekundu, madoadoa usoni, na mabega yake madogo

yaliyoinama ndani, huku amejifunga ngozi ya kondoo, Mungu alisema, "Huyo ndiye."

106 Maumbo yenu yote makubwa na kiburi haukumvutia Mungu. Unaweza kuwa D.D.D., Ph.D., au L. maradufu D. Unaweza ukawa askofu, papa, ama chochote unachoweza kuwa. Lakini inamhitaji Mungu kufanya kitu kutoka pasipo na kitu. Maadamu unaweza kuwa si kitu, Mungu ndiye hicho kitu Fulani. Maadamu unaweza kujiondoa njiani, basi Mungu anaweza kuingia. Lakini unapokuwa umejaa majivuno sana na ni mgumu, mpaka ukawa na makubwa kuliko yote na bora zaidi, huna chochote unachopaswa kuwa nacho: hicho ni moyo mnyenyekevu mbele za Mungu. Nasi tunajua hilo, ndugu. Bila shaka. Hakika.

107 Kamwe hukuona, au...kusikia jua likichomoza. Hukulisikia hilo. Je, umewahi kutoka nje, usiku, kusikia umande ukianguka? Tungefanya nini bila huo? Mnaona, haichukui huo.

108 Nitawaambia jambo moja sasa. Ni ninii tulivu...Maji yanayotiririka mbio ambayo yanafanya kelele nyingi namna hii, na kuruka juu-chini, siyo yanayoakisi uzuri wa nyota, ndani yake. Ni hicho kidimbwi kidogo kitulivu chenye kina kirefu, ndicho huakisi uzuri wa nyota.

109 Tunachohitaji, usiku wa leo, ni tukio hilo lenye kilindi, lililokolea, kitu hicho Fulani kilicho huko chini ndani yetu. Si—si lazima kipaze sauti, hata hivyo kinaweza. Lakini tunaweka mkazo wote kwenye kupaza kwetu sauti. Huenda kamwe kisinene kwa lugha, hata hivyo kinaweza. Lakini tunaweka mkazo wote juu ya hilo. [Sehumu tupu kwenye kanda—Mh.]

110 Huenda kisihudhurie mkutano wa Billy Graham, mkutano wa Oral Roberts, ama mkutano wangu. Si lazima uuhudhurie. Kinachopaswa kuwa nacho ni kina kile cha Upendo wa Milele wa Mungu. Huyo Roho aliye ndani yake, anayekufanya kile ulicho.

111 Hicho ndicho nilichokuwa nikizungumzia, asubuhi ya leo. Hicho ndicho nilichokuwa nikilivutia, Kanisa kuvuka Kalvari, huku na huko. Kamwe usifikiri kwamba kwa sababu umenena kwa lugha, au kwamba unajua mengi sana kuhusu Maandiko, ama umesoma vitabu vya mtu fulani, nawe unajua zaidi ya jamaa huyo mwingine. Alisema, "Tia alama juu ya wale wanaougua na kuomboleza kwa ajili ya machukizo yanayofanywa mjini." Angemtia nani alama katika miji yetu, usiku wa leo? Unaona, ni vilindi vya Roho, sio mambo ya juujuu. Si ganda lililo kwenye—kwenye kokwa la hikori lililo zuri. Ni kokwa la hikori lililo chini ya hilo ganda. Una ganda kubwa tupu. Huna kitu mle chini. Tunachohitaji, usiku wa leo, ni kilindi cha upendo wa Mungu.

112 Basi Eliya aliposikia Sauti hiyo ndogo tulivu, hakuna kitu kilichomsumbua.

113 Umesikia nini katika yote hayo? Utaondoka, katika siku chache. Ulimsikia Billy Graham. Utamsikia Oral Roberts.

Utawasikia wengine, watu wakuu. Sina neno dhidi ya watu hao; hao ni watumishi wa Mungu. Bali usisikilize hizo kelele. Isikilize hiyo Sauti ndogo tulivu, kilindi hicho cha kitu Fulani kinachoingia ndani ya moyo wa mwanadamu, kinachoondoa upumbavu wote kutoka kwako. Kinaondoa ulimwengu wote kutoka kwako. Kinakufanya uyachukie mambo ya ulimwengu na kuyapenda mambo ya Mungu. Hicho ndicho kilindi, hicho ndicho kidimbwi kinachoakisi nyota za utukufu wa Milele wa Mungu. Hicho ndicho kitu kinacholeta machozi machoni, kinacholeta furaha isiyosemeka, na iliyojaa utukufu. Kinakufanya usimame wakati mambo mengine yote yatakapokupungukia. Kinafanya . . . Ugonjwa unapokuja, au hata mauti yenyewe, bado kina uakisi wa baraka za Mungu ndani yake; kilindi hicho chenye kina kirefu, ndicho kinachoziakisi mbingu, sio hiyo mitiririko na kelele za maji. Maji yanayotiririka hayana kina kirefu sana. Maji matulivu ndiyo yenye kina kirefu.

114 Mungu na atusaidie, usiku wa leo, enyi marafiki, tunapoikaribia meza ya ushirika, kukumbuka hilo; haijalishi ni mambo gani tunayofanya kwa nje, ni mambo mangapi mazuri tunayofanya.

115 Unasema, "Vema, Ndugu Branham, mimi huhudhuria kanisa. Ninajaribu kuishi vizuri niwezavyo." Vema. Hakuna neno dhidi ya hilo, ndugu. "Nimenena kwa lugha, Ndugu Branham. Nimepaza sauti katika Roho." Hilo ni sawa. Ila hilo silo ninalozungumzia, ndugu. Hilo bado silo. Hilo silo ninalozungumzia.

116 Ninazungumza juu ya ile Sauti ndogo tulivu, kitu Fulani kile kilichokolea na kiaminifu. Ambapo, nilizoea kuwaona akina mama wa kale waliposhuka kwenye marefu haya ya kanisa hapa, miaka kadhaa iliyopita, machozi yakitiririka mashavuni mwao, wakati mvulana mmoja mwenye dhambi angesimama, kuja madhabahuni.

117 Siku hizi, ninatoa wito, na kumwona mvulana akija, wanaketi na kuzibua chingamu yao. Kuna nini? Umepoteza *kuisikia* hiyo.

118 Umesikia nini? Unasikia nini? Tuko kwenye wakati wa mwisho.

119 Mnasikia kwenye televisheni, na kwenye redio, katika magazeti yenu, kwenye magazeti yenu ya kila siku, ya kwamba kutakuwa na kimbunga kote katika nchi hii siku moja. Unasikiliza kwa ajili gani, kusikia hicho king'ora chote, umeifungulia redio yako, mchana kutwa, na upuuzi huo wote ukiendelea, kusikia wakati risasi zitakapodondoka, au mabomu? Mimi sisikilizi upuuzi huo.

120 Ninatega masikio nisikie Sauti ikisema, "Njoo huku juu. Ilikuwa vyema, mtumishi Wangu mwema na mwaminifu."

121 Unasikia nini? Unajua, nafikiri tunavutiwa sana kusikiliza kwa makini sana mambo yote ya ulimwengu, na mambo kama hayo, hatuwezi kusikia hiyo Sauti ndogo, tulivu.

122 Tunawasikia wachungaji wetu wakisema, "Jiunge tu na kanisa, itakuwa sawa." Tunasikia baadhi yao wakisema, "Nena tu kwa lugha, yote yamekwisha." Baadhi yao wanasema, "Piga kelele tu, yote yamekwisha."

123 Huwezi kusikia Sauti hiyo ndogo, tulivu ambayo huweka kitu Fulani kilichokolea na chenye kilindi maishani, hukufanya kile unachopaswa kuwa.

124 Ngano haizai ngano kwa sababu iko kwenye tawi au kwenye ubua. Gugu pia liko kwenye ubua. Lakini inahitaji uhai ulio katika hilo tawi kuchipusha ngano. Maji yanayoanguka juu yake yatainyweshea yote miwili. Yote miwili itafurahia ndani yake. Yote miwili itakulia ndani yake.

125 Wanaume na wanawake wanaweza kukua, wakipaza sauti na kumsifu Mungu, wakinena kwa lugha na kuwa wafuasi wa kanisa, wakicheza katika Roho na kutoa zaka, na bado kusiwe mioyoni mwao, na ile Sauti ndogo tulivu ya Mungu yenye upendo mwingi, na wenye kina.

126 "Nijapoutoa mwili wangu uchomwe kama dhabihu, wala sina upendo, si kitu mimi. Nijapotoa mali yangu yote kuwalisha maskini, ningali si kitu. Nina imani ya kuhamisha mlima, ningali si kitu mimi. Na—na—nanena kwa lugha, kama wanadamu na Malaika, ningali si kitu mimi." Mnaona? Ni ile Sauti ndogo tulivu inayonena ndani kabisa ya moyo wako, inayobadilisha kila mtazamo, inafanya tabia kuwa tofauti, nawe unakuwa kiumbe kipya katika Kristo.

127 Unasikia nini? Inategemea unachosikiliza, rafiki. Ikiwa unasikiliza, sikia . . . sio matamshi, sio uakisi, lakini kama unasikiliza, usikie juu ya uamsho mkuu mahali fulani, ambapo watu elfu kumi wamekusanyika, endelea; unasikiliza kitu kibaya. "Nitaenda kule nikajionee. Wanasema wana umati mkubwa." Hiyo haileti tofauti hata kidogo. Viwanja vya mbio vinao huo. Kila kitu kingine kinao. Roki zina huo.

"Ninaenda huko kwa . . . Ninaenda kule kwa ajili ya jambo lingine."

128 Kama ukienda kwa kitu kingine chochote isipokuwa . . . Kama unasikiliza kitu kingine chochote isipokuwa ile Sauti ndogo tulivu, rudi pangoni. Rudi chini ya mretemu, mpaka tuweze kujiandaa. Jishikilie kimya, na usubiri. Acha ngurumo zipite. Acha tetemeko la ardhi litikise. Acha upepo unaoenda kasi upite, nao moto uenee, chochote utakacho. Nauwazia wimbo ule:

Nifundishe, Bwana, jinsi ya kungoja wakati mioyo inawaka,
Jalia nidhalilishe kiburi changu, niliitie Jina Lako;
Dumisha kuifanya upya imani yangu, macho yangu yameelekezwa Kwako,
Acha niwe katika dunia hii jinsi unavyotaka niwe.

Hivyo ndivyo ninavyotaka kufanya.

Wale wamngojeao Bwana, watapata nguvu mpya,
Watapanda juu kwa mbawa kama tai,

Mnaamini hilo?

Watapiga mbio wala hawatachoka, watakwenda kwa miguu wala hawatazimia;
Nifundishe, Bwana, nifundishe, Bwana, jinsi ya kungoja.

129 Acha ngurumo zipite. Acha moto uenee. Lakini jalia nisikie Sauti ile ndogo tulivu, inayosema, "Njoni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo. Tokeni chini ya mretemu. Tokeni katika mapango yenu."

130 Ninataka kuifunika imani yangu, nikiikabili Damu Yake, nisonge mbele na kusema, "Naam, Bwana. Sasa naamini."

Na tuombe.

131 Ewe Bwana, Muumba wa mbingu na nchi, Mwanzilishi wa Uzima wa milele, na mpaji wa kila karama njema, uturehemu, Bwana. Sasa tunasimama tukiwa na haja ya kusikia. Sauti zetu, Bwana, zimepaa huko juu.

132 Na sasa tumesikia sauti nyingi sana. Kuna nyingi sana zisemazo, "Njoo huku kwenye kanisa *hili*. Laiti ungejiunga na kanisa letu! Tuna kundi bora zaidi jijini, watu waliovalia nadhifu zaidi. Meya wa jiji huenda kwetu."

133 Na watu wengi, katika mikutano yao, Bwana, wana magavana, na kadhalika, wa kuja na kutoa hotuba. Ee Mungu, niepushe nayo, Bwana. Nifiche pangoni na unijalie kungoja, Bwana. Ninajali nini yale gavana asemayo? Ninataka kusikia hiyo Sauti ndogo tulivu ya Mwokozi wangu. Loo, nisaidie kungoja, Bwana, na kufanya upya nguvu zangu ninapokungojea Wewe.

134 Pia ulisaidie kanisa hili, Bwana, wapate kukungoja Wewe, na ufanye upya imani yao, na kufanya upya nguvu zao, kupanda juu kama mbawa za tai. Jalia wawe wakisikiliza, Bwana, si zile kelele, sio yale mayowe, bali waisikilize ile Sauti ndogo tulivu.

135 Bwana, katika siku chache, ninapanda niingie pangoni kule, kusubiri. Ee Mungu, unisaidie, Bwana. Unipofushe, na uzibe

masikio yangu, na mambo ya ulimwengu, kwa ajili ya umaarufu, au kwa sifa, au kwa jambo lolote la bure ambalo ulimwengu huu ungeweza kutoa. Jalia nikae pale, Bwana, mpaka nitakapoisikia Sauti ile ndogo tulivu. Ndipo umjalie mtumishi Wako ajitokeze, Bwana, akipanda juu, juu ya mbawa za Tai. Tujalie, Bwana.

136 Libariki kanisa hili dogo. Mbariki Ndugu yetu Neville. Ondoa ugonjwa huo kwenye tumbo lake, Bwana, na uutupilie mbali naye. Mweke kazini, Bwana, na umruhusu arudi hapa, akiwa amefanywa upya. "Watafanya upya nguvu zao." Tujalie, Bwana.

137 Utusamehe dhambi zetu. Tunakuja kwenye meza ya ushirika sasa, Bwana. Ulisema, "Anayekula na kunywa hii isivyostahili, anakula na kunywa hukumu kwa nafsi yake, kwa kutokuupambanua mwili wa Bwana." Utusaidie, Bwana, kuzichunguza nafsi zetu, mioyo yetu. Na utujaribu uone kama kuna kitu chochote kichafu juu yetu. Kikiwepo, utusamehe, Ee Mungu, tunapokungojea Wewe kwa unyenyekevu. Tunaomba katika Jina la Yesu, Mwanao. Amina.

> Nifundishe, Bwana, kungoja, chini magotini mwangu,
> Na kwa wakati wako mzuri utajibu maombi yangu; (Hiyo ni kweli.)
> Nifundishe nisitegemee yale wafanyayo wengine,
> Bali kungoja katika maombi nipate jibu kutoka Kwako.

138 Hilo ndilo ninalotaka, jibu kutoka Mbinguni. Ninataka kuisikia Sauti Yake, si sauti ya meneja, si sauti ya meya, si sauti ya gavana, sio sauti ya askofu. Ninataka kusikia Sauti Yako, Bwana. Ule upole na unyenyekevu wa Roho Mtakatifu akizungumza moyoni mwangu, "Njoni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo." Naam, Bwana, tumeketi chini ya mretemu sasa. Tunangojea, tuone atasemaje.

139 Bwana amewabariki ninyi, kila mmoja, sasa. Ni wangapi wanaotaka kukumbukwa katika maombi? Hebu tuone ukiinua mkono wako. Useme, "Bwana, nifundishe kungoja. Nifundishe. Hebu ni—ni—nisahau kiburi changu chote. Wakati wengine wanapopita, wakifanya mambo makuu kama haya, jalia nidhalilishe kiburi changu, niliitie tu Jina Lako. Nifundishe kutotegemea yale wengine wafanyayo, lakini ningojee tu katika maombi jibu kutoka Kwako."

140 Kama Eliya alivyofanya. Alisubiri huko nyuma. Akasikia ngurumo. Akasikia radi. Akasikia kuporomoka kwa miamba. Akasikia moto. Akasikia upepo. Lakini hicho sicho alichokuwa akitazamia. Hata hakikumgusa nabii. Alikiacha kipite. Lakini wakati ile Sauti ndogo tulivu, alichukua vazi lake na kuliweka

juu ya uso wake, akaenda mwisho wa pango. Naye Bwana akasema, “Nenda, ukasimame juu ya mwamba kule chini.”

Hicho ndicho ninachotaka kusikia, “Simama juu ya mwamba.” Vema.

141 Ni wakati sasa wa ushirika. Bwana awabariki. Nafikiri, kwanza, kabla hatujafanya hili, tunataka kuomba dua kwa ajili ya kila mmoja humu ndani walioinua mikono yao, kwamba kweli walitaka Mungu awazungumzie. Je, kuna yeyote wenu hapa chini ya mretemu, usiku wa leo? Inua mkono wako. Hakika. Hakika, tuko. Wengi wenu hapa mko pangoni, mkingoja.

142 Mmeona mambo haya yote yakipita. Mlisikia uamsho mkuu wa Billy Graham, wa Oral Roberts, wangu mwenyewe, kila mahali pengine, Tommy Osborn, Tommy Hicks, hawa wote wakipita. Lakini iko wapi? Hiyo Sauti iko wapi?

143 Unasema, “Nimepiga makelele na akina Jessup. Nime—nimecheza katika Roho pamoja na Wanamuziki wa Harts. Nina mambo haya mengine yote. Nimefanya yote hayo. Lakini kiko wapi kitu hicho Fulani, Ndugu Branham, kinachonibania chini na kunitwika mzigo kwa ajili ya watu waliopotea, mpaka siwezi kupumzika kwa sababu yake?”

144 Sasa, hao ndio aina pekee watakaoingia. Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema. “Watie muhuri wale tu wanaougua na kulia kwa ajili ya machukizo yanayofanywa mjini.” Loo, hapo ndipo tunapoihitaji, marafiki.

Na tuombe tena.

145 Bwana! Tafadhali, Bwana! Loo, naweza nikaimba kupita kiasi. Huenda nikahubiri kupita kiasi. Huenda nikapaza sauti kupita kiasi. Huenda nikalia kupita kiasi. Lakini kamwe sitaomba kupita kiasi. Ee Mungu, nichunguze na unijaribu.

146 Nilikuwa tu nikizungumza, muda mfupi uliopita, kuhusu madimbwi ya kina kirefu, jinsi yanavyoziakisi nyota; tia kina cha Roho wako ndani yetu, Bwana, kama nabii Daudi alivyosema, “Uniongoze kando ya maji matulivu,” sio maji yanayotiririka. Maji matulivu, niongoze huko, Bwana. Ninyamazishe. Nina wasiwasi, nimechanganyikiwa sana.

147 Nimefanya kila kitu ulichoniambia nifanye, kadri nijuavyo mimi. Nimeenda kote katika taifa hili, kote ulimwenguni, nikihubiri, na kulia, na kushawishi. Umekuwa mwaminifu kutupa ishara hiyo ya Masihi, kuonyesha ya kwamba ni Wewe, Bwana, unayelifanya, wala si mwanadamu. Ninashukuru kwa ajili ya hilo. Lakini, Bwana, niko chini ya mretemu, usiku wa leo. Ninashangaa, “Kwa nini hawatubu? Kwa nini Marekani hii haiwezi kuliona, Bwana?” Je, hisia zake ni nzito hivi? Je, kanisa limeundiwa madhehebu, likabanwa sana? Wala hawatashirikiana. Hawatafanya chochote ila kukosoa.

148 Lakini nina hakika kabisa, usiku wa leo, kama ilivyokuwa kwa Eliya, chini ya ule mti, unao elfu saba, bado, ambao hawajapiga goti lao kwa Baalimu. Unao watakatifu wengi duniani leo, wanaongojea Kuja kwa Bwana.

149 Ee Bwana, uturehemu. Tujaribu, na ututie katika mizani yako ya kupimia. Na tukiona tumepatikana tumepungukiwa, Ee Bwana, tusafishe basi na dhambi zetu. Na utufanye vile Wewe ungetaka tuwe. Jalia hilo kwa kila mtu binafsi katika kanisa hili. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

150 Sasa itakuwa ni wakati wa ushirika. Tunaomba ya kwamba Mungu atawabariki sasa. Wote ambao hawana budi kwenda, wala hawataki kula ushirika, tukutane hapa Jumatano usiku, tutakuwa tukikutana tena.

151 Msisahau kuniombea. Nitayahitaji sasa. Katika siku chache zijazo, nitahitaji maombi. Sasa msilichukulie tu hivi hivi, bali niwekeni moyoni mwenu na kuniombea. Nahitaji maombi yenu. Nina maamuzi ya kufanya ambayo yanaweza kumaanisha tofauti ya mamilioni ya watu. Kitu fulani lazima kifanyike. Nimeenda kadiri niwezavyo, kwa nguvu zangu mwenyewe. I—inanibidi kupata ono kutoka kwa Mungu, kwa ajili yangu mwenyewe. Atanionyesha kwa ajili ya wengine, lakini si—sina budi kupata kitu kwa ajili yangu mwenyewe. Nakihitaji. Niombeeni. Atakituma iwapo mtaomba tu.

152 Nikiendesha gari huku, leo hii, nilikuwa nikitazama huku na huku. Nilikuwa huko nyumbani kwako, Ndugu Roy. Wala sikutaka kuingia; kulikuwa na gari limeegeshwa hapo nje. Nina deni la kuwatembelea wewe na Dada Slaughter. Mimi na Meda tulikuwa tukiendesha huko. Nikasema, "Vema, tutarudi baadaye kidogo," lakini nilishikwa na shughuli nyingi wala sikurudi. Tukizunguka, tukiendesha gari, barabarani, nikiwazia, "Ee Mungu, jambo fulani halina budi kufanyika. Sina budi kukushika Wewe mahali fulani."

153 Saa inakaribia. Gi—giza linaingia. Wakati wa mwisho umefika, dakika moja kabla ya usiku wa manane. Tazama uwepo wa adui, kule kutetemeka, hisia, hali ya wasiwasi, migogoro ya ulimwengu, na bila kujua kuwa hayo ndiyo maangamizi yako. Unaona? Loo, jamani! Hebu na tupande juu kwa mbawa kama tai, sasa, turuke kwenye mikono Yake aliye yeye yule jana, leo, na hata milele.

154 Sasa, wote wanaotaka kubaki kwa ajili ya ushirika, tutafurahi kuwa nanyi katika wakati huu wa ushirika.

155 Sasa, unayo Wakorintho wa Kwanza, naamini, mlango wa 11, pale. Nitakuomba ulisome sasa hivi, basi, Ndugu Neville, tafadhali. [Ndugu Neville anasoma Wakorintho wa Kwanza 11:23-32—Mh.]

[*Kwa maana mimi nalipokea kwa Bwana niliyowapa nanyi, Ya kuwa Bwana Yesu usiku ule aliotolewa alitwaa mkate:*]

[*Naye akisha kushukuru akaumega, akasema, Twaeni, mle: huu ndio mwili wangu, uliovunjwa kwa ajili yenu: fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu.*]

[*Vivyo hivyo akakitwaa kikombe, baada ya kula, akisema, Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu: fanyeni hivi kila mnywapo, kwa ukumbusho wangu.*]

[*Kwa maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo.*]

[*Basi kila aulaye mkate huu, na kukinywea kikombe hiki cha Bwana isivyostahili, atakuwa amejipatia hatia ya mwili na damu ya Bwana.*]

[*Lakini mtu ajichunguze mwenyewe, na hivyo aule mkate huo na kukinywea kikombe hicho.*]

[*Maana alaye na kunywa isivyostahili, hula na kunywa hukumu ya nafsi yake, kwa kutokuupambanua mwili wa Bwana.*]

[*Kwa sababu hiyo wako wengi kwenu walio dhaifu na wagonjwa, na wengi wamelala.*]

[*Kwa maana kama tungejihukumu wenyewe, tusingehukumiwa.*]

[*Ila tuhukumiwapo, twarudiwa na Bwana, isije ikatupasa adhabu pamoja na dunia.*]

156 Hilo halihitaji maelezo yoyote, ni hivi tu, "Tukila na kunywa isivyostahili, tunakula na kujinywea hukumu ya nafsi zetu wenyewe, kwa kutokuupambanua mwili wa Bwana. Kwa sababu hiyo wengi kwenu ni dhaifu na wagonjwa, na wengi wamekufa," mnaona, tunapokuja kula ushirika.

157 Kila Mkristo anapaswa kula ushirika. Ni wajibu wako. Ni pambano la kuamua. Unaona? Yesu alisema, "Usipoula, huna sehemu pamoja Nami." Unaona?

158 "Lakini alaye na kunywa isivyostahili hula na kunywea hukumu yake mwenyewe." Hiyo ni kusema, kama ungali uko nje pamoja na ulimwengu, na kufanya mambo ya ulimwengu, nao watu wakuone ukila ushirika, unakosea. Unajileletea tu fedheha. Nalo litakudhuru tu. Sio kwamba litamdhuru Mungu. Litakudhuru wewe. Na kwa hiyo mtu anapaswa kujichunguza.

159 Na kabla hatujakaribia wakati huu mtakatifu, wewe mwombe Mungu ayachunguze maisha yangu. Na kama nimefanya jambo lolote ambalo si sahihi, nisamehe hilo. Si—simaanishi kufanya hivyo. Nitalirekebisha kama atanifunulia.

Nami nitaomba jambo lile lile kwa ajili yenu. Kasema, "Mnapokutana, ngojeaneni." Hiyo ni kusema, "Ngojeaneni ninyi kwa ninyi, na kuombeana."

160 Tunataka kula ushirika huu. Na tusipofanya hivyo, hatuna sehemu Naye. Hivyo ndivyo alivyosema. Kwanza . . . Ama, Yohana Mtakatifu, mlango wa 6.

161 Sasa, hebu tuombe tu. Niombeeni, kimya kimya, huku mimi nikiwaombea.

162 [Ndugu Branham anaomba kwa sauti ya chini—Mh.] Ninaomba ya kwamba utatusamehe, kwa imani. Hebu Roho Wako, Ee Mungu, aje. Ninaomba ya kwamba utatusamehe makosa yetu yote kwa wanadamu . . . ? . . . samehe . . . ? . . .

163 Ee Bwana, yasikie maombi yetu. Haya ni maombi yetu ya msamaha, Bwana. Tunaomba msamaha. Tunaomba rehema. Utusamehe, Bwana. Kama ilivyoandikwa katika Neno Lako, "Utusamehe makosa yetu, kama sisi nasi tuwasameheavyo wanaotukosea. Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na uovu. Kwa kuwa Ufalme ni Wako, na nguvu, na utukufu, milele. Amina."

Naamini unazo nyingi sana . . .

UNAFANYA NINI HAPA? SWA59-0301E
(What Does Thou Here?)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili jioni, tarehe 1 Machi, 1959, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org